# Jarida la KILIMO

Toleo la Saba

ISSN: 1821-8113 Julai - Septemba, 2011



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe: Dkt. Ali Mohamed Shein wa pili kutoka kushoto pomoja na viongozi wengine akiwa katika harakati za uvunaji wa mpunga wa mbegu aina ya NERICA kituo cha uzalishaji wa mbegu Bambi, Wilaya ya Kati Unguja.*

## Yaliyomo

Maoni ya Mhariri/ Picha ya Jalada....Uk.2
Uvunaji na Uanikaji wa Karafuu....Uk.3 - 4
Upotevu wa Rutuba na Urutubishaji wa Ardhi....Uk.4 - 5
Uvunaji na Uanikaji wa Karafuu....Uk.6 - 7
Matukio katika Picha....Uk.8 - 9
Mabaraza ya Wakulima....Uk.10
Athari za Joto kwa Mifugo....Uk.11 - 12
Mbinu Bora za Ujasiriamali....Uk.13 - 14
Umuhimu wa Rasilimali za Msituni....Uk.15-16

## Bodi ya Wahariri

Washauri
Affan O. Maalim
Juma Ali Juma
Dk. Bakar S. Asseid

Mhariri Mkuu
Dk. Juma M. Akil

Msanifu na Mhariri Mtendaji
Hashim H. Chande

Wahariri Wasaidizi

Makame M. Abdulrahman

Nassor S. Mkarafuu

Nassor S. Mohammed

Mpiga chapa
Fatma A. Juma

Mpiga picha
Khamis A. Bakari

ANUWANI
Wizara ya Kilimo, Maliasili - Zanzibar
S.L.P. 159
Simu: +255 24 2230986
Fax: +255 24 2234650
E-mail: kilimo@zanlink.com
Tovuti: kilimoznz.or.tz

# MAONI YA MHARIRI

Ndugu wakulima, kupata chakula cha kutosha na kilicho bora kwa kila mwananchi ni suala gumu ambalo linahitaji mipango na mikakati mizuri ya serikali kupitia Wizara husika. Moja ya tatizo kubwa linalowakabili wananchi ni kuchelewa kukamilisha hatua za mwanzo za matayarisho ya mashamba, kulima eneo kubwa ambalo hawana uwezo nalo na kutokutumia zana na pembejeo bora za kilimo.

Ndugu wakulima, moja ya kikwazo kikubwa ni uwezo mdogo wa kutumia zana bora za kilimo, mbegu bora, mbolea na kutozingatia kanuni na taaluma bora za uzalishaji ambazo zinatolewa na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Vikwazo hivi humsababishia mkulima kutumia nguvu nyingi, muda mrefu na kupata mavuno hafifu na tija ndogo.

Ndugu wakulima, kwa miaka mingi neno “Ukulima wa Kisasa” limekuwa ni wimbo lakini bado mkulima wa visiwani anategemea zana na pembejeo duni kama vile mbegu na jembe la mkono (kijembe kongoroka). Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inafanya mabadiliko makubwa katika kilimo ili kukifanya kilimo hicho kiwe katika mfumo wa kisasa “Mapinduzi ya Kilimo”.

Ndugu wakulima, katika kufanikisha suala hili Serikali imeongeza upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo yakiwemo matrekta makubwa na madogo, mbegu bora na mbolea, kuongeza usamabazaji wa taaluma kwa wakulima kwa kuongeza idadi ya mabwana/mabibishamba katika shehia pamoja na kutoa ruzuku ya aslimia 75% kwa kazi za utayarishaji wa mashamba na ununuzi wa mbegu bora na mbolea.

Ndugu wakulima, hatunabudi kuunga mkono juhudi hizi za Serikali ili kufanikisha azma ya “Mapinduzi ya Kilimo” hivyo tunaipongeza na tunaiomba iendelee na juhudi zake za kuwashajiisha na kuwashirikisha wakulima kikamilifu katika kupanga malengo yao juu ya mpango wa utumiaji wa zana na pembejeo bora za kilimo.

Ndugu wakulima, kwa kuunga mkono juhudi hizi za Serikali, Wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea kutoa mafunzo ya utumiaji bora wa zana na pembejeo za kilimo na kuweka mpango maalumu ya mafunzo kwa kila shehia juu ya umuhimu wa zana hizo pamoja na matumizi yake ili kufikia lengo la wakulima katika kujitosheleza kwa chakula, kuinua hali zao za maisha na kuipunguzia mzigo Serikali wa kuagiza chakula kutoka nje ya nchi.

# PICHA YA JALADA

Katika picha anaonekana Rais wa Zanzibar Mhe. Ali Mohamed Shein akivuna mpunga wa mbegu aina ya NERICA katika shamba la kuzalisha mbegu liliopo Bambi pamoja nae kutoka kulia kwake ni Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe, Mansoor Y. Himid, Mkuu wa Mkoa wa Kusini (U) Mhe, Mustafa Ibrahim na Naibu Katibu Mkuu (kilimo) ndugu Juma A. Juma, tarehe 7 Julai 2011.

# ILI TUVUNE MAZAO BORA NI LAZIMA TUPANDE MBEGU BORA ZINAZOWEZA KUTUPATIA TIJA

Na Sabiha H. Saleh

Mnamo tarehe 2/7/2011 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein aliyasema hayo kwa nyakati tofauti aliposhiriki kikamilifu katika uzinduzi wa Kitaifa wa uvunaji wa mbegu ya mpunga aina ya "NERICA", huko Bambi na bonde la Kisima Mchanga liliopo Kiboje Mkwajuni Wilaya ya Kati Unguja.

Hii ni hatua mojawapo ya Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada zake za kukuza na kuendeleza kilimo kwa ujumla.

Dkt. Shein amesema kuwa lengo kuu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya mapinduzi ya kilimo tayari limeanza kutekelezwa na mbegu aina ya NERICA ndio mkombozi wetu kwani Serikali itaendelea kuchukua kila jitihada kuona kuwa wakulima wa Zanzibar wananufaika na kilimo chao pamoja na taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa azma ya Serikali kwa upande wake ni kuona kuwa Mapinduzi ya kilimo yanaleta tija kwa wakulima pamoja na wananchi kwa ujumla kwa kuweza kupata kile kilichokusudiwa.

Aidha, amefahamisha kuwa nia na dhamira ni kuwainua wakulima na Serikali inaendelea na taratibu za kuwaletea wakulima wake mashine za kuvunia mpunga, kuwapunguzia bei za pembejeo pamoja na kuwapatia matrekta kwa ajili ya kuvurugia na dawa za kuulia wadudu ili mkulima aweze kumudu gharama za uendeshaji na tuweze kulima kwa tija zaidi.

Akizungumzia kuhusiana na mfumko wa bei za vyakula hasa mchele ambao ndio chakula kikubwa kwa watu wa Zanzibar amesema kuwa Serikali tayari



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein aliyesimama na shuke la mpunga akiwa katika uzinduzi wa uvunaji wa mbegu ya mpunga aina ya NERICA katika Shamba la Uzalishaji wa mbegu Bambi

imeshaanza kutekeleza mapinduzi ya kilimo kwa kupambana na hali hiyo.

Akifafanua zaidi kuhusu ongezeko la Idadi ya Watu duniani, kwa upande wa Zanzibar amesema tokea Mapinduzi Matukufu ya Januari mwaka 1964 ambapo idadi ya watu ilikuwa 320,000 hadi mwaka 1974 ilikuwa ni 640,000 na kwa mujibu wa takwimu ya sensa ya mwaka 2002 ambapo ilifikia watu milioni 1.2 idadi ambayo inapelekea ongezeko la mahitaji ya chakula.

Kutokana na ongezeko la watu , takwimu zinaonyesha kwamba mchele unaotumiwa kwa chakula hapa Zanzibar ni tani 80,000 kwa mwaka, unaozalishwa na wakulima ni chini ya tani 16,000 na kiasi chote kilichobaki hununuliwa kutoka nje ya nchi. Aidha, Dkt. Shein alisisitiza haja ya kuongeza uzalishaji wa chakula.

Pia aliwataka wakulima kufuata ushauri wa watalamu na kubadilika ili kilimo chetu kiwe cha kisasa. Hivyo, hatuna budi kutumia teknolojia ya kisasa na kuweza kujitegemea katika kilimo cha mpunga kwa angalau asilimia 60, "Ukitumia mbegu bora unaweza kuvuna mavuno bora".

Amefahamisha kuwa kulima kwa kutumia mbegu bora kunapelekea kuvuna mazao mengi na bora, hivyo tuongeze jitihada na kukifanya chakula kuongezeka.

Aidha Dkt. Shein amesema kuwa Washirika wa Maendeleo wako tayari na wanaendelea na jitihada za kuiunga mkono Zanzibar katika Sekta ya Kilimo wakiwemo, Korea ya Kusini, Marekani, Japan hasa katika mradi wao wa 'Feed the Future'.

Akiwa katika bonde la Kisima Mchanga, Dkt. Shein aliwaahidi wakulima kuwajengea njia yao kwa kiwango cha kifusi kutoka barabara kuu hadi bondeni, kuwawekea umeme, kuwachimbia kisima na kuwapatia trela la kubebea mizigo.

Akimkaribisha Rais wa Zanzibar

Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid amesema kuwa Mapinduzi ya Kilimo ni mageuzi ya haraka yalioendelevu katika kukipa nguvu zaidi kilimo pamoja na wakulima kwani faida inayopatikana huwa ni kwa taifa zima.

Amefahamisha kuwa hali ya Ulimwengu imebadilika na sisi lazi tubadilike tuwe na mikakati imara katika kukibadilisha kilimo chetu kwa faida ya nchi yetu.

Alisema kuwa dhamira ya Wizara ya Kilimo na Maliasili ndani ya miaka mitano ni kulima hekta 6,000 za umwagijiliaji maji, kati ya hekta 8,521 ambapo kwa sasa ni hekta 700 tu ndizo zinazolimwa. Aidha, alifahamisha kuwa Jamhuri ya Korea ya Kusini imeahidi kusaidia kulima hekta 2,000 na Serikali ya Marekani hekta 2,000.

Aliongeza kusema kuwa mashamba darasa yataongezwa hadi kufikia 1,200, pia mashamba darasa manne ya mikarafuu yataanzishwa, mawili Unguja na mawili Pemba.

Mhe. Waziri wa Kilimo aliwaeleza wakulima kuwa katika bajeti ya Wizara ya mwaka 2011/2012 itakuwa na matumaini kwa wakulima wa visiwa hivi.

Nae Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja Mhe. Mustafa Muhammed Ibrahim aliwatoa hofu wakulima wa bonde la Kisimamchanga na kuwataka kuendelea kulitumia bonde hilo kwani tayari limeshapimwa na Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuanza kilimo cha umwagiliaji maji.

Nao wakulima wa bonde la Kisimamchanga wameushukuru mradi wa PADEP uliotumia zaidi ya shilingi milioni 32 ambao umeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza uzalishaji kutoka polo 4 kwa robo hekta kwa sasa, wakati hapo zamani walikuwa wakizalisha polo 4 kwa hekta nzima.

Jumla ya hekta 5 za mbegu ya mpunga wa aina ya 'NERICA' zimevunwa na zinatarajiwa kupandwa kwa wingi katika msimu wa mvua za vuli zijazo kwa lengo la kupandwa wakati wa masika ambapo zinatarajiwa zaidi ya tani 3,700 kupatikana katika msimu ujao wa masika ili kufikia asilimia 50% ya uzalishaji ndani ya miaka mitano.

Uzinduzi huo wa kitaifa uliwashirikisha viongozi kutoka Mikoa 5 ya Unguja na Pemba, wakiwemo Mawaziri, Wawakilishi, Mkuu wa Mkoa wa Kusini ambaye ndiye mwenyeji wa shughuli hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mjini/ Magharibi, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Viongozi wa Serikali pamoja na Wakisiasa na wananchi kutoka maeneo mbalimbali.

# UPOTEVU WA RUTUBA NA NJIA ZA KURUTUBISHA ARDHI

Na Hashim H. Chande

Ardhi yenye rutuba ni muhimu katika ukuwaji wa mimea na upatikanaji wa mavuno yaliyo bora. Kama tunavyoelewa kuwa rutuba ni chakula cha mimea ambacho kinapatikana kwenye udongo. Ili kuuweka udongo katika hali ya rutuba na kuiwezesha mimea iendelee kukua vizuri ardhini hatuna budi kutumia mbolea ili kurudisha chakula kilichochukuliwa na mimea.

Mbolea zinatumika kuongeza rutuba na kuiwezesha ardhi kutoa mazao mengi, kinachohitajika ni jinsi ya kujua aina gani ya mbolea, kiwango, na wakati zinapohitajika. Hivyo Mabwana/mabibi shamba waliomo katika maeneo ya kilimo wanajukumu la kuwaelimisha wakulima wa sehemu hizo.

**Tishio la upoteaji wa rutuba**



Ardhi iliyopoteza rutuba imeshambuliwa na ukame na hutoa mazao hafifu au kutoweza kutoa mazao ya aina yoyote.



Mchanganyiko wa vitu tofauti vilivyotumika katika kutengenezea mboji ikiwemo majani, udongo, takataka, mabaki ya mimea na maji.

**katika udongo**

Katika nchi yetu tumekabiliwa na tishio kubwa la kupoteza rutuba ya udongo kutokana uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji wa miti ovyo, kuchimba mchanga, kuchimba na kukata matofali ya mawe na kilimo kisichozingatia kanuni bora.

Ardhi inayotumiwa vibaya kwa kilimo pasi na kurudishia rutuba yake ni chanzo kikubwa cha upotevu wa rutuba hiyo ya asili ambayo ni chakula muhimu cha mimea na viumbe vyengine vinavyoishi katika udongo. Upungufu huo husababisha udongo kupunguza uwezo wake wa kuhifadhi maji kwa muda mrefu ambapo ukame hutokea na mazao yanayopandwa kutoa mavuno hafifu.

Rutuba hiyo ni lazima irudishwe ili tuweze kupata tena mavuno bora. Hivyo, tunapaswa kuzingatia urutubishaji wa ardhi kwa kuweka viwango sahihi vya mbolea kulingana na mahitaji halisi ya mimea iliyopandwa, kwa mfano mpunga unahitaji kiasi cha kilo 100 - 150 cha mbolea kwa kila ekari mbili na nusu (2.5). Kwa wale wakulima wenye tabia ya kupumzisha ardhi kwa kipindi cha mwaka mmoja au miwili kwa kuchunga wanyama au kuweka mazizi katika maeneo hayo wakati wa kupumzisha ardhi, njia hii husaidia kurudisha rutuba ardhini ijapokuwa hivi sasa haitumiki sana katika maeneo mengi kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya ardhi.

Kutokana na ongezeko la mahitaji ya matumizi ya mbolea za viwandani na gharama kubwa za upatikanaji wake, wakulima hatuna budi kujitengezea mbolea sisi wenyewe kwa kutumia malighafi tulizonazo kama vile kupanda mazao ya jamii ya kunde, matumizi mboji na samadi.

**UTENGENEZAJI WA MBOLEA YA MBOJI**

Ili kudumisha uzalishaji wa chakula, wakulima wa Zanzibar wanasisitizwa kutengeneza na kutumia mbolea ya samadi, mboji na takataka pale ambapo zinapopatikana kwa urahisi. Mbolea hizi mbali ya kurutubisha ardhi, pia husaidia kuifanya ardhi iwe katika hali nzuri iliyoshikamana. Ingawa wakulima wanahimizwa kutumia mbolea za viwandani kwa baadhi ya mazao, lakini sirahisi kufidia pengo la mbolea yote inayohitajika kwa wakati huu ambao ardhi inaonyesha kuchoka, kutokana na matumizi mabaya ya mfululizo. Kupuuza mbolea hizi kunaweza kuleta madhara makubwa katika kilimo.

Mbolea ya mboji ni mchanganyiko wa mabaki ya vitu vyenye asili ya uhai ambavyo hukusanywa kutoka mashambani na majumbani kama vile takataka, mabua ya mimea, magugu, vinyesi vya wanyama au hata mbolea ya chumvi chumvi.

**FAIDA YA MBOLEA YA MBOJI**

- Hukaa ardhini na hutumiwa na mimea kwa muda mrefu, kuliko mbolea ya chumvi.
- Mboji ina uwezo wa kubadili hali ya udongo na kuufanya utumike kwa kilimo.
- Mboji inawezesha udongo kuhifadhi unyevu kwa muda mrefu.
- Mboji ni rahisi kutengeneza, kutumiwa na haina gharama kubwa ukilinganisha na mbolea za viwandani.

**JINSI YA KUTENGENEZA**

i Safisha eneo unalotaka kutengeneza mbolea.
ii Pima mita 1.5 urefu na mita 1.5 upana na weka fito baada ya kupima urefu na upana, urefu wa fito unategemea mahitaji ya mkulima.
iii Chimbua chimbua na weka vizuri udongo.
iv Panga tabaka la udongo, majani, mabua na kuyatandaza pamoja na takataka zinazoweza kuoza.
iii Weka tabaka la udongo wa kutosha juu mabua na majani kwa mpangilio.
iv Tumia mbolea ya chumvi chumvi au vinyesi vya wanyama kwa kunyunyizia juu ya udongo.
v Nyunyizia maji baada ya kuweka mbolea, kwa kumalizia tabaka la kwanza. Rudia kuweka tabaka la pili mpaka la tatu juu yake kwa kufata mpangilio ule ule wa tabaka la mwanzo hadi kufikia urefu wa mita 1-2.
vi Hakikisha tabaka lina unyevu na joto la kutosha. Geuza tabaka hizo kila baada ya wiki mbili kwa kupunguza hewa na unyevu uliozidi ili kuozesha takataka kikalifu.
vii Mbolea hiyo inatakiwa itumike baada ya kuoza na kupoa.

# UVUNAJI NA UANIKAJI KARAFUU

Na Rashid Khamis

Zanzibar imekuwa ikijulikana sana katika uuzaji wa karafuu bora kuanzia karne ya 18, karafuu bora zinapatikana kutoana na uchumaji, uchambuaji, uanikaji bora pamoja na usafishaji wa karafuu kabla ya kuuza. Katika miaka ya 2000 tumeshuhudia kurejeshwa kwa uchafu wa karafuu zilizouzwa nje katika Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) Hali hii inasababisha Zanzibar kupoteza sifa yake ya kuuza karafuu bora.



Mwananchi akiwa katika harakati za kuvuna karafuu ili kuliokoa zao hili la kitaifa lisipotee

**UVUNAJI**

Karafuu nzuri kwa biashara ni yenye rangi kutoka kijani na kuingia rangi ya manjano kabla ya kuchanua. Karafuu ikachanua inabadilika na kuwa mbegu na hupoteza matumizi yaliyokusudiwa.
Wakati wa uchumaji wa karafuu ni vizuri kuepuka ukataji wa matawi kwani tabia hii hudhoofisha mikarafuu na husababisha kushambuliwa na maradhi na hatimae kufa.

Wakati wa kuchuma, matawi dhaifu ya mikarafuu mikubwa yafungwe pamoja kwa kutumia kamba. Aidha Hii itasaidia kufanya yawe madhubuti zaidi, hivyo kupunguza uwezekano wa kukwanyuka kutokana na uzito wa mchumaji. Kamba au vingoe vitumike kwa kuvuta matawi yaliyombali ili yaweze kuchumwa kirahisi badala ya kuyavunja. Mikarafuu midogo inaweza kuchumwa kwa kutumia ngazi na hii inasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu huo.



Mwanamama akiwa mstari wa mbele katika kushiriki kuchambua karafuu kwa lengo la kuliokoa zao hili la Taifa

**UANIKAJI**

Karafuu zianikwe haraka baada ya kuchambuliwa na kusafishwa na hakikisha sehemu za kuanikia zinapata jua wakati wote (kutwa nzima). Usianike karafuu karibu na jengo lolote au miti mirefu inayoweza kutoa kivuli.

Miongoni mwa vifaa vilivyo bora kwa kuanikia karafuu ni majamvi kwa sababu huhifadhi karafuu vizuri zaidi wakati wa mvua kuliko aina nyengine za vifaa kama magunia. Magunia yakiroa hufyonza maji na kurowesha karafuu, pia hupunguza gredi kwa kutoa nyuzi ambazo huchanganyika na karafuu.

Karafuu zinazoanikwa juu ya sakafu ziendelee kuwekwa kwenye majamvi kwa vile sakafu huchuna

karafuu wakati wa kugeuza na kuanua. Inashauria majamvi yawekwe juu ya majani mafupi kuepuka kuingia vumbi. Haitakiwi kuanika karafuu pembezoni mwa barabara ili kuepusha kupoteza ubora wake kwa kuchanganyika na vitu vengine, kupondwa na gari au kukanyagwa na wapita njia.

Karafuu bora zinatakiwa ziwe na sifa zifuatazo:

- Ziwe hazina vitawi, vijiti na matende nzima na zenye umbo la namna moja zisizoganda, hazina makonyo, mabegu, mpeta na takataka nyenginezo. Ziwe kavu kwa kiwango cha kukatika vipande viwili kwa kutumia vidole na zenye rangi ya zafarani.

Karafuu zina madini ya Calcium, Iron, Phosphorus, Sodium, Potassium, Hydrochloric acid, na vitamin A na C. Historia inatwambia kuwa katika karne ya tatu B.C, China iliweka sheria kuwa kabla ya kuzunguza na mfalme lazima kusafisha mdomo kwa kutumia karafuu. Aidha zaidi ya miaka 2000 iliyopita Wachina na Wahindi walizitumia karafuu kama viungo katika vyakula, dawa ya magonjwa ya meno na kuondosha harufu mbaya ya kinywa.

## MATUMIZI YA KARAFUU

### Madawa

Karafuu ina nguvu za kuponyesha magonjwa kama ifuatavyo:

- Mafuta ya karafuu yanatumika katika kuponyesha maumivu ya meno, vidonda vya ufizi na mdomo, hali hii imepelekea kuingizwa katika dawa za msuwaki na za kusukutuwa. Zinc huchanganywa na mafuta ya karafuu kwa kutibu meno yenye pango.
- Mafuta ya karafuu yakipakwa katika kidonda au mchubuko huzuwia maradhi ya "fungus" pia hupunguza maumivu baada ya kupaka sehemu ambayo umetafunwa na wadudu. Ngozi iliyopakwa mafuta ya karafuu huwa nyororo na huhifadhika na magonjwa. Hata hivyo, mafuta ya karafuu ni makali sana na yanahitaji kuzimuliwa.
- Mafuta ya karafuu yanachangamsha na kuondoa uchovu wa akili na mwili, upatikanaji usingizi ikiwa utakunywa kidogo pia hutumiwa katika kufanya masaji ambayo huondoa uchofu wa mwili.
- Mafuta ya karafuu yakichanganywa na chumvi na kupakwa kikomoni huondosha maumivu ya kichwa. Karafuu zikitafunwa husaidia kusafisha koo, kuponya kifua na pumu.
- Mchanganyiko wa mafuta ya karafuu na mafuta ya ufuta yakipakwa katika ngozi huponya magonjwa ya upele.
- Mafuta ya karafuu yanasaidia kusafisha damu, kuengeza mzunguko wa damu na kuengeza kinga ya mwiili.
- Mafuta na karafuu zinatibu maradhi ya tumbo.

Vipodozi, sabuni na mafuta mazuri.

- Mafuta ya karafuu (creams ) na mafuta ya kupaka (lotions) hulainisha ngozi na kuwa nyororo.
- Mafuta ya karafuu pia yanatumika katika kutengeneza mafuta mazuri.

### Sigara

Karafuu zinachanganywa na tumbaku na kutengenezwa sigara zenye ladha nzuri ya karafuu.

### Chakula

Karafuu inatumika kuongeza ladha katika vyakula kama pilau, uji, keki, "pudding" na "sausage". Unga wa karafuu unachanganjwa pamoja na unga wa viungo vyengine kutengeneza masala.



Karafuu zinahitaji kuanikwa katika maeneo yaliyosafi ili kuepuka kuchanganyika na takataka kwa lengo la kupata gredi iliyo bora

# Matukio ka



Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Mohamed Ali Shein akitia saini katika kitabu cha wageni baada ya kuzinduwa uvunaji wa mbegu ya mpunga aina ya NERICA katika Kituo cha Uzalishaji wa mbegu, Bambi.



Wakulima wa mpunga wa bonde la Mtwango r ya zana za kisasa ikiwemo matrekta madogo uburugaji wa mashamba ya mpunga.



Wakulima hujifunza zaidi mbinu bora za uzalishaji wa mazao wanapopata fursa za kushiriki katika ziara za kimafunzo ambapo hupata wasaa wa kudadisi pamoja na kubadilishana uzoefu walionao wao wenyewe katika kuendeleza kilimo.



Upandaji wa mikoko katika maeneo ya pwani mazingira ya pwani yaliyoharibiwa kutokana r tatizo la kuharibika fukwe na kupanda maji katil

# atika Picha



na Bumbwisudi wako mbele katika matumizi (Power tiller) katika kazi za uchimbuaji na




Wafanyakazi wa Kitengo cha Utibabu wa Mimea wakiwa katika kazi za kuweka dawa ya kunasia nzi wa matunda katika mitego maalum ili kukabiliana na tatizo hilo ambalo linarudisha nyuma juhudi na maendeleo ya wakulima katika kukuza zao la matunda.



ni njia moja wapo ya kutunza na kudhibiti na ukataji ovyo wa mikoko ili kukabiliana na ka maeneo ya kilimo..



Wizara ya Kilimo na Maliasili katika juhudi zake za kukuza kilimo cha umwagiliaji maji inaendelea kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkuu wa Taifa wa Kilimo cha Umwagiliaji maji kwa lengo la kwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji na tija.

# MABARAZA YA WAKULIMA NI CHACHU YA MAENDELEO YA KILIMO ZANZIBAR

Na Shauri Haji

Mabaraza ya wakulima (Farmers Fora) yaliyoanzishwa miaka minne iliyopita katika wilaya tisa za Unguja na Pemba na Programu za Kuimarisha Huduma za Kilimo na Maendeleo ya Mifugo (ASSP na ASDP-L) Zanzibar ni vyombo muhimu vya kuwaunganisha wakulima ingawa dhana hii ni ngeni katika visiwa hivi.

Mabaraza hayo ya wakulima yameanzishwa katika Wilaya ya Magharibi, Kati, Kusini, Kaskazini A na Kaskazini B, kwa upande wa Unguja na Wilaya ya Mkoani, Chake chake, Wete na Micheweni kwa Pemba.

Mabaraza hayo licha ya kuwa na changangamoto za kiutendaji tangu yaanzishwe, yamekuwa ni chachu kwa maendeleo ya kilimo na mifugo sambamba na kuwa na sauti ya kumtetea mkulima. Hata hivyo, bado kuna dhana kwamba programu za ASSP na ASDP-L ndizo zenye jukumu la kugharamia ma baraza hayo.

Dhana ya kuanzishwa kwa Mabaraza ya Wakulima imekuja baada ya kuona ipo haja kwa wakulima kuwa na chombo chao cha kuwaunganisha ili waweze kutatua matatizo yao kwa pamoja, kuzijua haki zao na kuzitetea. Tangu kuanzishwa kwa mabaraza hayo wakulima wameweza kutatua migogoro yao ya ardhi hasa katika maeneo yaliyo nje ya utekelezaji wa miradi ya ASSP na ASDP-L.

Katibu wa Baraza la wakulima la Wilaya ya Kati Unguja Bi Mashavu Juma Mapuri ambae pia ni katibu wa skuli ya wakulima (FFS) ya Mwera Kichaka Mabuzi, alisema kwamba wakulima katika shehia mbali mbali wanaamini kuwa hiki ni chombo pekee kinachotumika kupata taarifa na ushauri kuhusu maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo, kuwatetea, kuwasemea na kushawishi kuhusu haki zao na kuwa na sauti ya pamoja ya kufikisha maoni na matatizo yao bila woga kwa wahusika.

Alifahamisha juhudi kubwa zilichukuliwa kuwashajiisha wakulima kutoka shehia nyengine kujiunga na chombo hicho na kuondoa dhana potofu miongoni mwa wakulima kwamba Mabaraza hayo ni kwa ajili ya shehia zinazotekeleza miradi iliyo chini ya programu za ASSP na ASDP-L na kwamba wakulima wa



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansor Yussuf Himid aliyesimama akiwa anasisitiza mshikamano wa wakulima wakati akizungumza na wajumbe wa Mabaraza ya Wakulima huko Dunga Wilaya ya Kati, Unguja.

shehia nyengine hawahusiki. Hali hiyo imewajengea imani wakulima na kuweza kufuatilia kwa karibu taarifa katika Mabaraza ya Wakulima.

Mabaraza hayo yaliundwa kwa lengo la kujenga mashirikiano ya karibu na watoa huduma binafsi na kuwajengea uwezo wakulima kitaaluma na kuwawezesha kuongeza uzalishaji wenye tija na kupunguza umasikini na kuongeza kipato. Mabaraza haya kwa kawaida huwa na wanachama 20 akiwemo Mwenyekiti, Katibu na Mshika fedha pamoja na wajumbe 17 kwa kila baraza la Wilaya.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuwatembeza wakulima 50 wa muhogo na mazao mengine katika kikundi cha “Nguvu Kazi Tusizembee” cha Kisongoni wilaya ya Kaskazini ‘A’ kinachojishughulisha na ukulima wa mpunga ambapo wakulima hao walipata maelezo, kuhamasika na kuanzisha kilimo cha mpunga katika maeneo yao. Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Baraza la Wakulima la Wilaya ya Kaskazini A nd. Abeid Ussi Haji.

Waziri wa Kilimo na Maliasili, Zanzibar Mhe, Mansoor Yussuf Himid akizungumza na Baraza la Wakulima la Wilaya ya Kati, Dunga amekuwa na imani kubwa na Mabaraza hayo yaliyoanzishwa Unguja na Pemba. Aidha, aliwaeleza wakulima Serikali ya awamu ya saba inayoongozwa na Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein imekusudia kuleta mageuzi makubwa katika kilimo kwa kupunguza gharama za pembejeo muhimu kwa asilimia 75% zikiwemo mbolea, mbegu, madawa, gharama za kuchimba na kuburuga ili kumwezesha mkulima kumudu gharama hizo.

Waziri amelihakikishia baraza la wakulima kwamba Wizara yake inakusudia kuimarisha miundombinu ya masoko, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na kujenga barabara ndogo zinazoingia mashambani kwa kuziunganisha na barabara kuu ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya wakulima.

Aidha, aliwahakikishia wakulima kuwa mbegu mpya ya mpunga aina ya NERICA inayoota katika maeneo ya juu itazalishwa na kusambazwa kwao ili waweze kuzalisha zaidi. Wastani wa tani 140 za NERICA zinatarajiwa kuzalishwa ili kila mkulima aweze kutumia mbegu bora kutoka asilimia zero hadi kufika asilimia 33.6.

# ATHARI YA JOTO KWA MIFUGO

Na Nassor S. Mohammed

Hali ya hewa inajumuisha ujoto, unyevu wa hewa, mvua, upepo, miale ya jua, uzito wa hewa pamoja na mazingira yote katika maeneo husika. Kwa kawaida hali ya ujoto na mvua huwezesha mimea na mifugo kuishi na kukua vizuri.

Mifugo ni miongoni mwa viumbe ambavyo hutegemea sana hali ya hewa katika kuishi na kuzalisha mazao kama maziwa, nyama, mayai, manyoya na ngozi ambavyo hutumiwa kwa chakula, kutengeneza makoti ya baridi, mikanda, mikoba na masofa. Wanyama hawa wanahitaji hali ya hewa ambayo ni nzuri kwa ajili ya kuishi na kuzalisha pindi ikikosekana athari zake hujitokeza.



Kuku wa mayai wanahitaji joto la wastani ili waweze kula na kunywa maji kwa wingi, hali ambayo huchangia zaidi katika utagaji wa mayai.

Kwa kawaida wanyama wakubwa wanahitaji joto lenye nyuzi joto kati ya 37 - 40 sentigredi na wadogo wanahitaji joto la mwili kati ya nyuzi joto 40- 44 sentigredi, mfano:

Ng'ombe...............38.5$^{0}$C
Kondoo.................38.0$^{0}$C– 39.5$^{0}$C
Mbuzi...................40$^{0}$C
Farasi...................38$^{0}$C
Mbwa...................39$^{0}$C
Paka......................38.5$^{0}$C
Sungura................39.3$^{0}$C
Kuku......................42.1$^{0}$C
Bata.......................21$^{0}$C



Mifugo kama ng'ombe hukuwa vizuri zaidi na kutoa maziwa kwa wingi ikiwa itawekwa katika maeneo ambayo yana kivuli na kupitisha hewa ya kutosha.

Mifugo inapokuwa na joto jingi katika miili yao, mara nyingi hutoa jasho na mwili hupoteza joto hilo na akihisi baridi huzuia utoaji wa jasho na ujoto hubaki mwilini.

**Malisho**

Hali ya hewa huchangia katika uimarikaji wa malisho, ulaji na ukuaji wa mifugo. Mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kondoo wanapokuwa machungani ikiwa hali ya hewa ni ya joto kali hushindwa kutembea na kujitafutia chakula pia malisho huwa hafifu. Hivyo mifugo hukosa chakula cha kutosha na kushiba. Ng'ombe wa kienyeji wanaweza kustahamili hali ya joto ukilinganisha na ng'ombe wa makabila ya nchi za baridi au machotara.

Hali ya ubaridi huimarisha malisho na huiwezesha mifugo kutumia muda mwingi machungani kujipatia chakula zaidi badala ya kukaa kivulini. Ng'ombe na mbuzi wa kabila za kigeni, mfano Friesian,

Jersey na Saanen, Norwegian na machotara huhitaji chakula kingi zaidi wakikosa huathirika.

Katika nchi za joto kuna vipindi vya mvua nyingi ambapo mimea hukua haraka na kupea mara moja. Kwa kawaida mifugo hula kidogo sana majani yaliyokomaa hata kama itakuwa na njaa kwa sababu majani hayo yana desturi ya kutoa joto jingi yanaposagwa mwilini hivyo, joto jingi husababisha mifugo kutoweza kula vizuri chakula hicho kwa manufaa ya miili yao na uzalishaji.

**Vyakula vya ziada**

Mbali na majani, vyakula vyengine vya ziada kama vile mabaki ya vyakula vilivyoliwa na binadamu, maganda ya muhogo, viazi, magomba, masalia ya mashambani, pumba, mashudu na madini yanahitajika kulishia wanyama. Vyakula hivi ambavyo hupunguza na havitoi joto jingi mwilini ni vizuri kupewa wanyama hasa mifugo ya kabila za nchi za baridi na machotara ambao kwa kawaida wanahitaji chakula kingi. Vyakula vya mifugo vinatakiwa viweze kupoza joto la mwili yaani vyenye protini. Ng'ombe huacha kula kabisa wakati mwili wake ukiwa na joto kali.

**Maji**

Maji ni muhimu sana katika ukuaji na uzalishaji wa mifugo na mazao yake hivyo mifugo inahitaji maji kwa sababu kuu mbili:

Maji ni chakula na ni sehemu ya mwili wao. Maji hupoza joto la mwili linalotokana na usagaji na matumizi ya chakula katika kiwiliwili.

Joto linafanya mifugo inywe maji mengi, kwa ng'ombe wa kigeni wa maziwa mwili ufikapo nyuzi joto 29.4 sentigredi unywaji wa maji hupungua na kusababisha ulaji wa chakula kuwa mdogo hivyo kuathiri uzalishaji.

Mifugo iliyozoea maeneo na mazingira yake hunywa maji kidogo ukilinganisha na ile ambayo ni wageni katika eneo hilo mfano kutoka kwenye baridi kuja kwenye joto na mvuke mwingi hewani huifanya mifugo inywe maji mara kwa mara.

**Utoaji wa maziwa**

Joto kali husababisha uzalishaji wa maziwa kuwa mdogo na kuharibika kirahisi. Ng'ombe wa kigeni kama Jersey na Friesian wanatoa maziwa mengi katika mazingira ya baridi lakini joto likizidi njuzijoto 10 sentigredi ng'ombe hawa hupunguza maziwa na ifikapo nyuzijoto 21 hadi 27 sentigredi, utoaji wa maziwa hushuka kwa kiwango kikubwa.

**Uzazi**

Joto, unyevu wa hewani na mwangaza unachangia katika kiwango cha uzalishaji wa mifugo. Joto jingi mwilini linaharibu mbegu za uzazi za kike na za kiume pamoja na mayai ambayo yamepandishiwa yakiwemo katika harakati za kufanya mtoto. Vizazi vinavyozaliwa nyakati za joto kali na kutohifadhiwa katika mazingira mazuri hufa kwa urahisi. Aidha, joto kali linapunguza utagaji wa mayai kwa jamii ya kuku.

**Maradhi**

Hali ya joto inachangia kuishi, kukua na kuzalisha vimelea na viumbe vinavyosababisha maradhi kwa mifugo. Mifugo ya makabila ya kigeni huathiriwa kirahisi na kupata maradhi. Mazingira mazuri, shibe na maji husababisha mifugo kukua haraka, kuwa na afya nzuri na kuweza kuhimili maradhi.

**Mazao ya mifugo**

Mazao mengi ya mifugo, mfano maziwa, nyama na mayai huharibika haraka yakiwekwa katika hali ya joto. Ndugu wafugaji inafaa kuchukua tahadhari ya kutunza mazao hayo katika maeneo yenye baridi, pia tunaombwa tutayarishe malisho kwa ajili ya wakati wa kiangazi ili wanyama wetu wapate malisho bora na kuongeza uzalishaji.



Mbuzi wa maziwa pia wanahitaji mabanda yaliyoinuka, yenye kupitisha hewa na mwanga wa kutosha ili waweze kukua vizuri na kutoa maziwa kwa wingi.

# MBINU BORA ZA UJASIRIAMALI

Na Haji A. Omar

Ujasiriamali ni uwezo wa kumudu na kuendesha biashara kwa faida katika mazingira ya ushindani sokoni, uhaba wa mtaji na bila ya kujali hasara nyengine.

**Mjasiriamali ni nani?**

Ni mtu ambaye ana maono ya biashara, mwenye uwezo wa kugundua fursa, mwenye msukumo wa kukusanya rasilimali na kuthubutu kuanzisha mradi kwa imani kwamba atafanikiwa katika biashara yake.

**Sifa kuu za Mjasiriamali:**

- Mwenye kutafuta fursa
- Anaetimiza makubaliano katika biashara
- Mwenye utashi wa ubora na ufanisi katika kazi yake
- Mwenye malengo ya muda mfupi na muda mrefu
- Mwenye uwezo wa kupanga na kusimamia kazi yake
- Mwenye ari ya kutafuta habari
- Mwenye uwezo wa kushawishi na kutoa ushirikiano
- Anaejiamini na kutenda

Ijapokuwa watu wengi husema kwamba uwezo wa kijasiriamali ni kipaji cha kuzaliwa na huthubutu kufananisha na baadhi ya makabila yanayofanikiwa kibiashara kama vile, Wakikuyu-Kenya, Wahindi na Waarabu-Asia, Wachaga-Tanzania Bara na Wapemba-Zanzibar. Watu wengine husema Ujasiriamali unapatikana kwa kusomea, Je nani yuko sahihi kati ya wenye hoja mbili hizi?

Utafiti uliofanywa sehemu tofauti duniani haukubaliani na hoja ya kwanza pekee, kuwa mjasiriamali hamilikiwi na kundi fulani pekee



Mjasiriamali anaweza kuekeza katika biashara yoyote ile bila ya kujali kutokea kwa hasara, kinu cha kusagia nafaka ni moja ya biashara hizo.

katika jamii bali mjasiriamali anaweza kutoka katika kabila na jamii yoyote duniani. Vile vile watalamu wengi wanakubaliana kwamba Mjasiriamali akiwa na sifa zote mbili ndio muamala zaidi kuliko kuwa na kipaji cha kuzaliwa pekee.

Kila mtu anaweza kuwa mjasiriamali, cha muhimu ni kuamua, kujituma na kutenda. Baadhi ya wataalamu wanasema hakuna mtu anaezaliwa mjasiriamali, bali watu wengi huiga au kujifunza ujasiriamali kutoka kwa waliowazunguka kama vile wazazi, walezi au kupitia mafunzo ya fani hiyo. Kwa mantiki hiyo, yeyote anaweza kuwa mjasiriamali na mwenye mafanikio makubwa ya kupigiwa mfano.

**USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA BIASHARA ZA KILIMO**

Biashara za kilimo
Zinajumuisha utaratibu mzima wa kupangilia matumizi ya pembejeo za kilimo ili kuweza kudhibiti na kutambua uhusiano baina ya pembejeo zilizotumika na mazao yaliyopatikana katika kipindi cha uzalishaji. Utaratibu huu unahusiana na kuelewa uchumi wa kilimo na mbinu za ujasiriamali katika kumudu na kuendesha miradi midogo na mikubwa.

**Usimamizi na uendeshaji**

Ni utendaji wa kazi kwa kutumia mtu au kikundi cha watu pamoja na rasilimali nyingine kwa utaratibu maalum uliopangwa ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kazi za usimamizi na uendeshaji ni pamoja na kupanga, kuongoza, kuhamasisha, kuajiri, kudhibiti na kutathmini.

**Mambo muhimu ili msimamizi aweze kufanya kazi zake vizuri:**

- Awe mwenye kuielewa kazi yake vizuri
- Atoe au kupata motisha
- Afuate taratibu za sheria
- Awe mwenye kufahamu mazingira ya kazi
- Awe na uwezo wa kufanya

tathmini ya kazi

**Sifa za mjasiriamali katika kusimamia biashara:**

1. Kuweka malengo kwa usahihi na yawe mahsusi, yanayopimika, yanayofikika, yanayofaa na yanayoweza kufuatiliwa.

2. Kuwa na mfumo wa taarifa na kuweka kumbukumbu kama vile kudhibiti na kutathmini maendeleo, kufanya maamuzi na kupanga mipango ijayo, kuelewa mbinu mpya juu ya teknolojia, masoko na mazingira.

3. Muda ni bidhaa muhimu kuliko bidhaa nyengine na kama muda hautunzwi hakutakua na maendeleo mazuri. Muda ni kigezo kikuu cha utendaji ukitunzwa huleta ufanisi.

Kutunza muda ni kugawa muda huo kwa ajili ya kuweka malengo kwa umuhimu wake, kugundua na kuondosha vipoteza muda na kutumia maarifa ya uongozi ili kufikia malengo kiufanisi zaidi.

**Mambo ya kuzingatia:**

- Hakuna namna ya kuweza kufidia muda – Dakika moja iliyopotea haiwezi kurudi tena

- Panga mambo yako kwa vipaumbele ili kuokoa muda

- Hakuna muda mchache, kuona muda mchache ni dalili za uongozi mbaya

- Kulala wakati wa usiku ni njia pekee ya kupumzika na sio kucheza gemu au kukaa maskani wakati wa mchana kama ndio njia muafaka ya kupumzika

Mambo yafuatayo husababisha mtu kupoteza muda bila kujijua au kwa kujua kwa maana ya kupumzika:

- Kucheza gemu na kuandika ujumbe wa maandishi sana katika simu

- Kupokea na kufurahia wageni wanaokuja bila miadi

- Kutoweka malengo na vipaumbele vya kazi

- Kucheza karata, draft na bao la kete wakati wa kazi

- Dawati lililojaa karatasi bila mpango

- Kutogawa kazi kikamilifu au kufanya kazi zinazoweza kufanywa na walio chini yako

- Kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja

- Kushindwa kusema hapana au siwezi

- Ukosefu wa nidhamu

4. Motisha ni kitu chochote kinachohimiza juhudi katika kazi. Kwa kawaida binaadamu akipata motisha huongeza juhudi. Vifuatavyo ni vitu vitolewavyo ili kuongeza juhudi:

   - Motisha kwa wafanyakazi ni kama vile kumpandisha cheo, kupata bonasi yanapotokea mafanikio makubwa na ongezeko la mshahara

   - Motisha kwa wateja ni kama vile kupunguza bei, usafiri wa bure, nyongeza ya kitu juu ya bidhaa aliyonunua, huduma nzuri kwa mteja ukiwemo ukarimu na uchangamfu.

5. Mawasiliano kwa mjasiriamali ni njia pekee ya kupokea habari kwa haraka, husaidia wateja kuelewa huduma, biashara au bidhaa zitolewazo na kupokea maoni ya wateja. Usipoitangaza biashara yako na kutafuta taarifa itakua vigumu kuingia katika ulimwengu wa biashara, kama vile usemi maarufu usemavyo "BIASHARA ITANGAZWAYO NDIO ITOKAYO"

Zipo njia tofauti za mawasiliano zinazotumiwa na wajasiriamali. Miongoni mwake ni :

- Mawasiliano kwa maandishi kama vile mabango ya matangazo, barua, vipeperushi, ripoti, lebo za kwenye bidhaa humuwezesha mjasiriamali kuwasiliana na wateja wake au wadau wengine wa biashara.

- Mawasiliano kwa njia ya maongezi kupitia mijadala, warsha, kongamano, semina na mikutano. Mjasiriamali anaweza kupata muda mzuri wa kuwasiliana na wateja kwa kushiriki kwenye mafunzo ya shamba darasa, sehemu za maonyesho ya bidhaa kama vile maonesho ya biashara na ya wakulima

- Mawasiliano ya ishara kama vile ishara za uso, mikono, mabega na kichwa, njia hii hutumika kwa wateja au wadau wengine wa biashara mara nyingi njia hii hutoa ujumbe mzuri au mbaya. Hivyo mjasiriamali lazima awe makini na ishara atoazo mteja hata kama wateja wanawasiliana wao wenyewe wanapokuwa katika eneo la biashara.

# UMUHIMU WA RASILIMALI ZA MSITUNI

Na Nassor S. Mkarafuu

Rasilimali za msituni zina uasili wa kibaiolojia zikijumuisha wanyama na mimea ya aina na rika tofauti yenye faida kwa maisha ya viumbe pamoja na huduma zinazopatikana msituni au ardhi inayotumika. Kuwepo kwa rasilimali hizi kunategemea uwepo wa msitu.

Rasilimali za msituni zina faida nyingi kwa maisha ya viumbe wakiwemo binadamu, wanyama na wadudu. Miongoni mwa faida za moja kwa moja ni upatikanaji wa chakula, miti ya mapambo, vichanganyisho vya manukato, mbegu pamoja na upatikanaji wa wanyama na mimea yenye kutoa tiba.

Faida nyengine ni pamoja na uhifadhi wa vyanzo vya maji, kurekebisha hali ya hewa, ufyonzaji wa hewa mkaa, uhifadhi wa udongo na kuzuia mmong'onyoko, ambapo katika nchi nyingi za Afrika, rasilimali hizi zina umuhimu wa upatikanaji wa lishe kwa kaya.

## UTEGEMEZI WA JAMII KWA MAZAO YAPATIKANAYO MSITUNI

Duniani kote jamii zinategemea rasilimali zinazopatikana msituni ikiwemo kujikimu kwa chakula, malisho ya wanyama, madawa na zana za ujenzi. Matumizi mengine ni pamoja na kupatikana zana za ukulima, utengenezaji wa mapambo ya majumbani.

Nchi nyingi za Afrika na Asia, jamii hutegemea rasilimali hizo kwa kuongeza kipato cha kaya, kupata uhakika wa chakula na lishe, biashara na ajira kwa ujumla. Hata hivyo rasilimali hizo hazipewi umuhimu na wanasiasa na wapangaji wa mipango ya Maendeleo licha ya umuhimu wake, mara nyingi watu hutoa thamani ya msitu pale tu yanapopatikana mavuno yake, kuyatumia, kutengeneza bidhaa, kuziuza na kuchangia kuoengeza kipato kwa jamii za vijijini. Rasilimali hizi ni kiashirio kikubwa katika kupunguza umasikini kwa jamii zinazotegemea msitu kwa kuongeza kipato, kupata uhakika wa chakula.



Misitu huchangia katika upatikanaji wa rasilimali nyingi pamoja na umuhimu wake husaidia katika kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji.

### Uhakika wa Chakula na Lishe

Rasilimali za msituni zina mchango mkubwa katika kuchangia uhakika wa chakula na lishe katika jamii kwa nyanja tofauti kama vile kupata chakula kinachochangia kutoa vitamini, madini, uanga na protini muhimu. Jamii nyingi za vijijini zinatumia vyakula vinavyopatikana msituni kwa kula au kuuza kwa lengo la kupata pesa za kununulia chakula hasa wakati wa uhaba wa mavuno ya mazao mashambani. Miongoni mwa mazao yanayopatikana msituni ni pamoja na matunda, mboga mboga, wanyama pori na asali.

### Matunda

Mabungo, Zambarau, Fuu, Ukwaju, Ubuyu, Mapera, Pilipilidoria, Maviru, Kunazi na Chongoma. Aidha, katika baadhi ya nchi za Afrika mazao kama edible nuts zinatumika kwa chakula, mafuta ya kula, viungo, achari na vinywaji.

### Mbogamboga

Miongoni mwa mboga zinazopatikana ni kikwayakwaya, pwipwi, mchicha mwiba, mchunga, mronge, mchambale, mboga ya pwani na mnavu. Aina hizi za mboga za asili zinatoa madini mengi zaidi kuliko aina ya mboga zisizokuwa za asili. Inasemekana mboga za asili zina madini ya chokaa (calcium) 1.5 – 3.2 zaidi ya mboga mboga za jamii ya kabeji ambazo ndizo zenye madini ya chokaa (calcium) nyingi kwa mboga zisizokuwa za asili.

### Wanyama pori

Wanyama pori ni miongoni mwa chakula muhimu katika kuongeza uhakika wa chakula na lishe wakijumuisha wanyama, ndege na mayai yao pamoja na samaki. Nyama itokanayo na wanyama hawa ni chanzo cha protini na madini mengine kama chuma, vitamin A na B. Wanyama wadogo (paa) na ndege (kanga) ni maarufu katika kuongeza chakula na lishe ya jamii.

### Asali

Ni miongoni mwa chakula maarufu hapa nchini. Kawaida asali iliyo nyingi hutengenezwa na nyuki na hupatikana msituni baada ya

// Jarida la KILIMO

Toleo la Saba

Julai - Septemba, 2011

kuvunwa ambayo hutumika katika jamii kwa kula, dawa na biashara. miongoni na Faida nyengine, masega ya nyuki hutumika katika kutengeneza mshumaa na maji maji yaitwayo royal jelly.

Matumizi ya asali yanatofautiana kutoka sehemu moja hadi nyengine kutokana na upatikanaji na hali ya soko. Wananchi wa vijijini mara nyingi hutumia asali kama dawa ya kutibu maradhi mbali mbali pamoja na kuuza kwa kujiongezea kipato. Hapa Zanzibar lita moja inauzwa kwa wastani wa shilingi 12, 000. Hii inamaanisha kwamba asali ni moja kati ya rasilimali yenye umuhimu katika afya na kuongeza kipato katika jamii.




Kima punju ni miongoni mwa rasilimali ya msituni ambayo ni kivutio kikuu cha Msitu wa Hifadhi wa Jozani kwa watalii wa ndani na wa nje ya nchi.

**Dawa za asili**

Dawa za asili ni mazao muhimu yanayopatikana kutoka msituni ambapo nchi zote za Afrika zinatumika. Zaidi ya watu bilioni 3.5 wanaoishi pembezoni mwa misitu duniani wanatumia dawa za asili na inakisiwa aina 35,000 zinatumika ambapo katika nchi za Afrika zaidi ya asilimia 80 ya watu wanatumia dawa za asili kwa matibabu ya maradhi na maumivu mbali mbali. Shirika la Afya Duniani (WHO) limekisia kwamba zaidi ya asilimia 80 ya watu katika nchi zinazoendelea wanategemea dawa za asili kwa matibabu ya msingi na zinapatikana kwa urahisi na jamii inazifahamu.

Miongoni mwa miti ya dawa maarufu zinazotumika hapa nchini ni pamoja na Mchofu, Mvuje, Mtarawanda, Kivumbasi, Mwavikali na Mpande ambazo zinatumika kwa kutibu maradhi mbali mbali kwa binadamu yakiwemo maradhi ya tumbo, kichwa, ngiri pamoja na maradhi ya matumbo ya kinamama.

**Miti ya mapambo**

Miti hii inatumika maalumu kwa ajili ya mapambo katika maeneo inayoishi jamii na kupendezesha hali ya mandhari. Jamii nyingi zinatumia miti hii katika nyumba zao au katika sehemu ambazo watu hupenda kupumzika na kwenye mahoteli za kitalii. Miongoni mwa miti maarufu inayotumika kwa mapambo inayopatikana msituni ni pamoja na Mgwede, Mkonge, Mkuyu na Mnunu ambayo pamoja na kutumika kwa mapambo pia hutumika kwa kutoa kivuli.

**Uhifadhi wa vyanzo vya maji**

Maji ni rasilimali za misitu zinazosaidia uzalishaji wa bidhaa mbali mbali na kuongeza pato la taifa na yanasaidia kwa afya ya binaadamu. Maji ya mito, maziwa, mvua na sehemu za unyevu ni vyanzo muhimu vya uzalishaji wa mazao. Misitu inasaidia kuhifadhi kina cha maji, kupatika kwa uhakika na kupunguza chumvi katika maji. Aidha, miti inatoa nafasi ya makaazi ya samaki. Majani na magogo yalioza yanaongeza virutubisho kwa viumbe waishio majini.

Rasilimali zinazopatikana msituni ni muhimu na zinahitaji kuwekewa mkakati maalum wa kuziendeleza na kuzitunza kwa vile zinachangia kustawisha uchumi wa nchi kwa kuongeza pato la taifa na usitawi wa maisha ya mwanadamu pamoja na viumbe vyengine. Aidha, taasisi zinazohusika ni vyema kufanya utafiti na kuweza kuzitangaza rasilimali hizi na kuzianisha kwa jamii na matumizi yake.

GAZETI HILI HUTOLEWA KILA BAADA YA MIEZI MITATU NA
WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI - ZANZIBAR
P. O. Box 159 Zanzibar, Simu: +255 24 2230986, Fax: +255 24 2234650
Barua pepe: kilimo@zanlink.com, Tovuti: www.kilimoznz.or.tz